HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO.
(*Barua zote zitumwe kwa Mkuu wa Shule)*

MKOA WA ARUSHA
Simu.*Namba . 0754486342*

Shule ya Sekondari Loliondo
S.L.P 61,
LOLIONDO.

Kumb Na. LSS/S.1005/J/2/VOL I/23 **17/12/ 2023.**

NDUGU: _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KWA MWAKA 2024

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga katika Shule ya Sekondari LOLIONDO.
Ninakupongeza kwa kubahatika kuchaguliwa kwako na unakaribishwa na Uongozi wa Shule. Unatakiwa kuitumia nafasi hii vizuri kwa kusoma kwa bidii na kufanya kazi zote kwa kujituma kwa wakati wote uwapo hapa shuleni kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kufuata kanuni, sheria na taratibu za shule. Hali ya hewa ni ya baridi kwa muda wote wa majira ya mwaka mzima.

2. KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa tarehe 08/01/2024 hadi tarehe 22/01/2024 (Ndani ya siku kumi na Nne) na masomo yataanza rasmi tarehe 23/01/2024, ni vema uwepo siku hiyo. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni. Shule ipo Wilayani Ngorongoro, Tarafa ya Loliondo, Kata ya Orgosorok, Kijiji cha Wasso. Yapo mabasi ya kutoka Arusha, Karatu, Ngorongoro hadi Loliondo. Wewe teremkia Wasso – Standi na kuelekea upande wa Magharibi umbali mita 800 mahali shule ilipo.

3. VIFAA VYA KUJA NAVYO SHULENI

i. Baadhi ya vifaa unavyatakiwa kununua na kuja navyo siku ya kuripoti ni:

- Daftari 15 na kalamu za kutosha (Counter book Quire 3). Madaftari madogo hayatakiwi.
- Rula 1
- Mathematical set 1
- Vyombo vya kulia chakula (Sahani, Kikombe, Bakuli na Kijiko) viwe vya mfupa au udongo. Vyombo vya plastic na bati haviruhusiwi.
- Toilet paper za kutosha kwa matumizi binafsi

Vifaa hivi vyote hapo juu pia vinapatikana katika duka la shule.

- Four figure table 1
- Rim paper (A4) kwa matumizi binafsi
- Dictionary Oxford – English to English

- Begi la kubebea madaftari na vitabu (Mifuko ya aina yoyote ni marufuku kuonekana nayo hapa shuleni).
- Uje na sanduku la chuma (trunk) lililo imara na kufuli imara.
- Viatu vyeusi vya kamba visivyokuwa na visigino virefu pea mbili (2)
- Uje na ndoo ya maji ya lita 20. kwa matumizi binafsi.
- Mwanafunzi aje na **fagio (chelewa), jembe lenye mpini, Fyekeo, ufagio laini wenye mpini (Soft broom)** kwa ajili ya usafi wa mazingira
- Uje na Godoro la sponchi la futi 2½ upana na blanketi zito.

4. SARE ZA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kushona sare za shule na sare za nje ya darasa na ambazo hazibani mwili kama ifuatavyo;

1. **WASICHANA**

A. **Sare za darasani**

- Sketi rangi NYEKUNDU (**Red)**
- Suruali ya lastick (belt) rangi NYEKUNDU
- Sweta rangi NYEUSI
- Socks nyeupe - jozi 2
- T-shirt 2 za rangi ya LIGHT BLUE (Bluu Bahari) ZENYE NEMBO YA SHULE (T – shirt hizo zinapatikana duka la shule kwa bei ya shilingi elfu kumi (**Tsh. 10,000/=** kwa T – shirt moja)
- Shati JEUPE mikono mifupi (2)
- Tai — rangi NYEKUNDU

B. Sare nje ya darasa (Shamba dress isiyobana)

- Sketi na suruali rangi KAKI
- Tracksuit rangi ya LIGHT BLUE (Bluu Bahari) yenye mistari meupe pembeni .
- Sock NYEUSI za michezo - jozi 2
- Raba nyepesi NYEUSI.

❖ **Shuka 2 za rangi ya Pink au Blue bahari**

ZINGATIA -Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa amevalia sare ya shule aliyoshonewa na sio nguo ya nyumbani.

2. **WAVULANA**

A. Sare za darasani (Zisibane mwili wala zisiwe- "MNYONYO"

- Suruali rangi NYEUSI **(Black)** (lazima ziwe na marinda mbele na mfuko wa nyuma uwekwe kifungo).
- Sweta rangi NYEKUNDU
- Socks NYEUPE - jozi 2
- T-shirt 2 za rangi ya LIGHT BLUE (Bluu Bahari) ZENYE NEMBO YA SHULE (T – shirt hizo zinapatikana duka la shule kwa bei ya shilingi elfu kumi (**Tsh. 10,000/=** kwa T – shirt moja)
- Shati JEUPE lenye mikono mifupi – 2

- Tai - rangi ya NYEUSI

B. **Sare nje ya darasa (Shamba dress)**

- Suruali rangi ya KAKI lazima ziwe na marinda mbele na mfuko wa nyuma uwekwe kifungo).
- Tracksuit rangi ya LIGHT BLUE (Bluu Bahari) yenye mistari meupe pembeni .
- Socks NYEUSI - jozi 2
- Raba nyepesi rangi NYEUSI.

❖ **Shuka 2 za rangi ya Pink au Blue bahari**

ZIINGATIA -Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa amevalia sare ya shule aliyoshonewa na sio nguo ya nyumbani.

5. MAMBO YA KUZINGATIA

- Hairuhusiwi kumiliki simu ya mkononi, ni kosa kubwa ukikutwa nayo unafukuzwa shule mara moja.
- Hairuhusiwi kuwa na mavazi tofauti na sare za shule.
- Hairuhusiwi kuwa na vifaa vya muziki (Radio).
- Shule haina utaratibu/uwezo wa kutoa chakula maalumu (Special diet) kwa wanafunzi wenye matatizo ya kiafya ila hutoa chakula laini pale tu mwanafunzi anapougua na kulazwa hospitali zilizopo karibu na shule.
- Hairuhusiwi kuonekana nje ya eneo la mipaka ya shule isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka ofisi ya malezi.
- Hairuhusiwi kuwa na vitu vingine vya thamani mbali na ulivyoelekezwa kwenye fomu hii. (Fedha za matumizi zikabidhiwe ofisi ya malezi).
- Uwe na fedha za matibabu binafsi endapo umeugua.
- Unashauriwa kufungua akaunti benki ya NMB kuhifadhi fedha binafsi za matumizi

6. MUHIMU

- Unatakiwa upimwe kwenye hospitali ya Serikali kuthibitisha afya yako. Tumia fomu iliyo ambatanishwa.
- Ili kupokelewa unatakiwa kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa hapo juu.
- Baadhi ya sheria za shule zimeambatishwa uzisome, uzielewe na uzisaini.
- Rejesha fomu ya Hospitali ikiwa imekamilika na Sheria, Kanuni na Taratibu za shule zikiwa zimesainiwa na Mzazi/Mlezi na mwanafunzi.
- Mwanafunzi aje na Bima ya Afya. Kama mzazi si mfanyakazi wa Serikali mtoto akatiwe Bima ya **CHF ILIYOBORESHWA** au **TOTO CARD.**
- Siku za kuja kuwaona / kuwasalimia wanafunzi ni Ijumaa na Jumamosi ya mwisho wa mwezi, siku zingine hutaruhusiwa kumuona mwanafunzi.

KARIBU SHULE YA SEKONDARI LOLIONDO

_____

NEEMA G. MCHAU

MKUU WA SHULE

Nakala: -

1. Mkurugenzi Mtendaji,
   Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro,
   S.L.P 1,
   LOLIONDO.
2. Afisa Elimu Sekondari,
   Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro,
   S.L.P 1,
   LOLIONDO.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

(Fomu hii irejeshwe siku ya kuripoti shuleni).

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima.
- Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
- Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapokuwa shuleni.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- Kuwa na mavazi ya heshima, mavazi ya nyumbani na mitepesho hairuhusiwi kwa mwanafunzi.

Makosa yatakayoweza kusababisha kufukuzwa shule mara moja.

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile, uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli, ugoro n.k.
v. Kupigana au kupiga.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii. Kudharau Bendera ya Taifa.
viii. Kuoa au kuolewa.
ix. Kutoa mimba.
x. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
xii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

Mimi _____ mzazi/mlezi wa_____.
Ninaahidi kwa hiyari yangu kuwa nitampa mtoto wangu mahitaji kulingana na sheria, kanuni na taratibu za Shule. Aidha nitatumia muda huu ninapomwandaa mtoto wangu kumuelekeza kuhusu kujitahidi na masomo awapo shuleni.

Saini ya Mzazi Tarehe

_____ _____

SEHEMU HII IJAZWE NA MTOTO

Mimi _____ nimekubaliana na sheria kanuni na taratibu zote za Shule, na ninaahidi kuwa nitazingatia na kuzifuata kama nilivyoagizwa. Naahidi kuwa nitasoma kwa bidii sana ili kuwa na matokeo mazuri.

Saini ya Mzazi Tarehe

_____ _____

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

TO: The Medical Officer,

……

……

……

Mr & Mrs/Miss

……

Please examine the above name as to his/her fitness mentally and for a full time Secondary Education. The examination should include the following categories: (i-iii) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of a defect.

Pregnancy (category iv) will also render a girl candidate in eligible for the Secondary Education.

i. (a) Eye-Sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech
(e) Venereal Diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy

ii. Neuroses

iii. Other serious

iv. Pregnancy

Date: …… **Signature:**

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Gov. Office)

PART B

I have examined the above name and consider that he/she is physically and mentally fit/unit for full time Secondary Education.

i. (a) Eye-Slight …… (b) Hearing ……
(c) Limbs …… (d) Speech ……
(e) Venereal Diseases …… (f) Epilepsy ……
(g) Leprosy ……

ii. Neuroses ……

iii. Other Serious diseases ……

iv. Pregnancy ……..

Date …… Signature …… Design ……